*Yohana 1:29, 10-13 (NENO)*

# Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!... wale waliaminio jina lake

---

**Siku iliyofuata, Yohana alimwona Yesu akimjia akasema, “Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu! ... Huyo Neno alikuwako ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kupitia kwake, haukumtambua. Alikuja kwa walio wake, lakini wao hawakumpokea. Bali wote waliompokea, aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake. Hawa ndio wasiozaliwa kwa damu, wala kwa mapenzi ya mwili au kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 3:3, 14-17 (NENO)*

# Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee... kupitia kwake ulimwengu upate kuokolewa

---

**Yesu akamjibu, “Amin, amin nakuambia, hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu kama hajazaliwa mara ya pili.” ... Kama vile Mose alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu. Ili kila mtu amwaminiye awe na uzima wa milele. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Kwa maana Mungu hakumtuma Mwanawe kuuhukumu ulimwengu, bali kupitia kwake ulimwengu upate kuokolewa.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 7:24, 37-39, 43 (NENO)*

# Yeyote aniaminiye mimi… vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake



Acheni kuhukumu mambo kwa jinsi mnavyoona tu, bali hukumuni kwa haki.” … Siku ile ya mwisho ya Sikukuu, siku ile kuu, wakati Yesu akiwa amesimama huko, akapaza sauti yake akasema, “Kama mtu yeyote anaona kiu na aje kwangu anywe. Yeyote aniaminiye mimi, kama Maandiko yasemavyo, vijito vya maji ya uzima vitatiririka ndani mwake.” Yesu aliposema haya alimaanisha Roho Mtakatifu ambaye wote waliomwamini wangempokea. … Kwa hiyo watu wakagawanyika kwa ajili ya Yesu.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 6:33, 35, 37, 63 (NENO)*

# Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu... Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima

---

**Kwa maana mkate wa Mungu ni yule ashukaye kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima." ... Yesu akawaambia, "Mimi ndimi mkate wa uzima. Yeye ajaye kwangu, hataona njaa kamwe na yeye aniaminiye, hataona kiu kamwe. ... Wale wote anipao Baba watakuja kwangu na yeyote ajaye kwangu, sitamfukuzia nje kamwe. ... Roho ndiye atiaye uzima, mwili haufai kitu. Maneno haya niliyowaambia ni Roho tena ni uzima.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 11:35-36, 38; Marko 14:33-36 (NENO)*

# Tazama jinsi alivyompenda Lazaro!... si kama nipendavyo mimi, bali vile upendavyo wewe

---

**Yesu akalia machozi. Ndipo Wayahudi wakasema, "Tazama jinsi alivyompenda Lazaro!" ... Yesu kwa mara nyingine akiwa amefadhaika sana, akafika penye kaburi. ... Kisha akawachukua pamoja naye Petro, Yakobo na Yohana. Akaanza kuhuzunika sana na kutaabika. Akawaambia, "Moyo wangu umejawa na huzuni kiasi cha kufa. Kaeni hapa na mkeshe." Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba kwamba kama ingewezekana saa hiyo ya mateso imwondokee. Akasema, "Abba, Baba, mambo yote yawezekana kwako. Niondolee kikombe hiki. Lakini si kama nipendavyo mimi, bali vile upendavyo wewe."**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 13:14-17, 20 (NENO)*

# Imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea ninyi… mtumishi si mkuu kuliko bwana wake

---

**Kwa hiyo, ikiwa mimi niliye Bwana wenu na Mwalimu wenu nimewanawisha ninyi miguu, pia hamna budi kunawishana miguu ninyi kwa ninyi. Mimi nimewawekea kielelezo kwamba imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea ninyi. Amin, amin nawaambia, mtumishi si mkuu kuliko bwana wake, wala aliyetumwa si mkuu kuliko yule aliyemtuma. Sasa kwa kuwa mmejua mambo haya, heri yenu ninyi kama mkiyatenda. … Amin, amin nawaambia, yeyote anayempokea yule niliyemtuma anipokea mimi, naye anipokeaye mimi ampokea yeye aliyenituma mimi.”**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 14:6, 9, 19; 10:9-11 (NENO)*

# Mimi ndimi njia na kweli na uzima... kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai

**Yesu akawaambia, "Mimi ndimi njia na kweli na uzima. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia kwangu. ... Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu yeyote aliyeniona mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, 'Tuonyeshe Baba'? ... Bado kitambo kidogo ulimwengu hautaniona tena, ila ninyi mtaniona, kwa kuwa mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai. ... Mimi ndimi lango, yeyote anayeingia zizini kwa kupitia kwangu ataokoka, ataingia na kutoka, naye atapata malisho. Mwizi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao tele. "Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 15:1-2, 4-5 (NENO)*

# Kaeni ndani yangu… Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa ndani ya mzabibu

**“Mimi ndimi mzabibu wa kweli na Baba yangu ndiye mkulima. Kila tawi ndani yangu lisilozaa matunda, Baba yangu hulikata, nalo kila tawi lizaalo, hulisafisha ili lipate kuzaa matunda zaidi. … Kaeni ndani yangu, nami nikae ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda lisipokaa ndani ya mzabibu, vivyo hivyo ninyi msipokaa ndani yangu hamwezi kuzaa matunda. “Mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi. Akaaye ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana, maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya jambo lolote.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yohana 17:3-6 (NENO)*

# Uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma



**Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Nimekutukuza wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye. Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja na wewe kabla ulimwengu haujakuwepo. “Nimelidhihirisha jina lako kwa wale ulionipa kutoka ulimwengu. Walikuwa wako, nawe ukanipa mimi, nao wamelitii neno lako.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Marko 4:14-20 (NENO)*

# Udanganyifu wa mali na tamaa ya mambo mengine huja na kulisonga lile neno



Yule mpanzi hupanda neno. Hawa ndio wale walio kando ya njia ambako neno lilipandwa. Walisikiapo neno, Shetani huja mara na kulinyakua lile neno lililopandwa ndani yao. Nazo zile mbegu zilizoanguka kwenye udongo wenye miamba, ni wale wanaolisikia neno, na mara hulipokea kwa furaha. Lakini kwa kuwa hawana mizizi, wao hudumu kwa muda mfupi tu. Kisha dhiki au mateso yanapoinuka kwa ajili ya lile neno, mara wao huiacha imani. Lakini wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye miiba, hulisikia lile neno; lakini masumbufu ya maisha haya, na udanganyifu wa mali na tamaa ya mambo mengine huja na kulisonga lile neno na kulifanya lisizae. Wengine, kama mbegu iliyopandwa kwenye udongo mzuri, hulisikia lile neno, wakalipokea na kuzaa mazao. Wao huzaa mara thelathini, au mara sitini, au mara mia ya mbegu iliyopandwa."




*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Marko 11:22-25 (NENO)*

# Mwaminini Mungu... sameheni mkiwa na neno na mtu

**Yesu akawajibu, "Mwaminini Mungu. Amin, nawaambia, mtu yeyote atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini,' wala asione shaka moyoni mwake, bali aamini kwamba hayo asemayo yametukia, atatimiziwa. Kwa sababu hiyo nawaambia, yoyote mtakayoyaomba mkisali, aminini ya kwamba mmeyapokea, nayo yatakuwa yenu. Nanyi kila msimamapo kusali, sameheni mkiwa na neno na mtu, ili naye Baba yenu aliye mbinguni awasamehe ninyi makosa yenu. [**



***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 3:10-15 (NENO)*

# Kila mmoja inampasa awe mwangalifu jinsi anavyojenga... hakuna mtu yeyote awezaye kuweka msingi mwingine wowote isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, ambao ni Yesu Kristo... moto utapima ubora wa kazi ya kila mtu

---

**Kwa neema Mungu aliyonipa, niliweka msingi kama mjenzi stadi na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mmoja inampasa awe mwangalifu jinsi anavyojenga. Kwa maana hakuna mtu yeyote awezaye kuweka msingi mwingine wowote isipokuwa ule uliokwisha kuwekwa, ambao ni Yesu Kristo. Kama mtu yeyote akijenga juu ya msingi huu kwa kutumia dhahabu, fedha, vito vya thamani, miti, majani au nyasi, kazi yake itaonekana ilivyo, kwa kuwa Siku ile itaidhihirisha. Itadhihirishwa kwa moto, nao moto utapima ubora wa kazi ya kila mtu. Kama kile alichojenga kitabaki, atapokea thawabu yake. Kama kazi kitateketea, atapata hasara, ila yeye mwenyewe ataokolewa, lakini tu kama mtu aliyenusurika kwenye moto.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 3:5-7, 21-23 (NENO)*

# Mungu ndiye aliikuza... mtu asijivune kuhusu wanadamu... ninyi ni wa Kristo

Kwani, Apolo ni nani? Naye Paulo ni nani? Ni watumishi tu ambao kupitia wao mliamini, kama vile Bwana alivyompa kila mtu huduma yake. Mimi nilipanda mbegu, Apolo akatia maji, lakini Mungu ndiye aliikuza. Hivyo mwenye kupanda na mwenye kutia maji si kitu, bali Mungu peke yake ambaye huifanya ikue. ... Hivyo basi, mtu asijivune kuhusu wanadamu! Vitu vyote ni vyenu, ikiwa ni Paulo au Apolo au Kefa au dunia au uzima au mauti, au wakati uliopo au wakati ujao, haya yote ni yenu na ninyi ni wa Kristo, naye Kristo ni wa Mungu.

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Wakorintho 4:4-7 (NENO)*

# Ngojeni mpaka Bwana atakapokuja... kuweka wazi nia za mioyo ya wanadamu... kwa nini mnajivuna kama vile hamkupokea?



**Dhamiri yangu ni safi, lakini hilo halinihesabii kuwa asiye na hatia. Bwana ndiye anihukumuye. Kwa hiyo msihukumu jambo lolote kabla ya wakati wake. Ngojeni mpaka Bwana atakapokuja. Yeye atayaleta nuruni mambo yale yaliyofichwa gizani, na kuweka wazi nia za mioyo ya wanadamu. Wakati huo kila mmoja atapokea sifa anayostahili kutoka kwa Mungu. Basi ndugu zangu, mambo haya nimeyafanya kwangu binafsi na Apolo kwa faida yenu, ili mweze kujifunza kutoka kwetu maana ya ule usemi usemao, "Msivuke zaidi ya yale yaliyoandikwa." Hivyo hamtajivunia mtu fulani na kumdharau mwingine. Kwa maana ni nani aliyewafanya kuwa tofauti na wengine? Ni nini mlicho nacho ambacho hamkupokea? Nanyi kama mlipokea, kwa nini mnajivuna kama vile hamkupokea?**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*2 Wakorintho 10:3-5, 17-18 (NENO)*

# Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu... tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo



---

**Ingawa tunaishi duniani, hatupigani vita kama ulimwengu ufanyavyo. Silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu, na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo, ... Lakini, “Yeye ajisifuye na ajisifu katika Bwana.” Kwa maana si yeye ajisifuye mwenyewe akubaliwaye, bali yeye ambaye Bwana humsifu.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*2 Wakorintho 5:4, 10, 17, 20-21 (NENO)*

# Kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya

---

**Kwa kuwa tukiwa bado katika hema hii twalia kwa uchungu na kulemewa, kwa sababu hatutaki kuvuliwa bali kuvikwa makao yetu ya mbinguni ili kwamba kile kipatikanacho na mauti kimezwe na uzima. … Kwa kuwa sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apate kulipwa kwa ajili ya yale ambayo yametendwa katika mwili wake, yakiwa mema au mabaya. … Kwa hiyo kama mtu akiwa ndani ya Kristo, amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita, tazama, yamekuwa mapya. … Kwa hiyo sisi ni mabalozi wa Kristo, kana kwamba Mungu anawasihi kupitia kwa vinywa vyetu. Nasi twawaomba sana ninyi kwa niaba ya Kristo, mpatanishwe na Mungu. Kwa maana Mungu alimfanya yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu kwake yeye.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Wagalatia 3:2-3; 5:1, 4, 13-14 (NENO)*

# Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru... msitumie uhuru wenu kama fursa ya kufuata tamaa za mwili

---

**Nataka nijifunze neno moja kutoka kwenu: Je, mlipokea Roho wa Mungu kwa kushika sheria, au kwa kuyaamini yale mliyosikia? Je, ninyi ni wajinga kiasi hicho? Baada ya kuanza kwa Roho, je, sasa mwataka kumalizia katika mwili? ... Kristo alitupa uhuru, akataka tubaki huru. Hivyo simameni imara wala msikubali tena kulemewa na kongwa la utumwa. ... Ninyi mnaotafuta kuhesabiwa haki kwa njia ya sheria mmetengwa na Kristo, mko mbali na neema ya Mungu. ... Ndugu zangu, ninyi mliitwa ili mwe huru, hivyo msitumie uhuru wenu kama fursa ya kufuata tamaa za mwili, bali tumikianeni ninyi kwa ninyi kwa upendo. Kwa maana sheria yote hukamilika katika amri moja: "Mpende jirani yako kama nafsi yako."**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Wagalatia 5:16-17, 19-24 (NENO)*

# Enendeni kwa Roho... tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu

**Kwa hiyo nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa maana mwili hutamani yale yaliyo kinyume na Roho, naye Roho hutamani yale yaliyo kinyume na mwili. Roho na mwili hupingana na kwa sababu hiyo hamwezi kufanya mnayotaka. ... Basi matendo ya mwili ni dhahiri nayo ni haya: Uasherati, uchafu, ufisadi, kuabudu sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi na mambo mengine yanayofanana na hayo. Nawaonya, kama nilivyokwisha kuwaonya kabla, kwamba watu watendao mambo kama hayo, hawataurithi Ufalme wa Mungu. Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Katika mambo kama haya hakuna sheria. Wote walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili na shauku zake pamoja na tamaa zake.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Timotheo 2:1-6 (NENO)*

# Dua, sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote... ili tupate kuishi kwa amani na utulivu, katika uchaji wote wa Mungu na utakatifu



**Awali ya yote, nasihi kwamba dua, sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote: kwa ajili ya wafalme na wale wote wenye mamlaka, ili tupate kuishi kwa amani na utulivu, katika uchaji wote wa Mungu na utakatifu. Jambo hili ni jema, tena linapendeza machoni pa Mungu Mwokozi wetu, anayetaka watu wote waokolewe na wafikie kuijua kweli. Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani mwanadamu Kristo Yesu, aliyejitoa mwenyewe kuwa fidia kwa ajili ya wanadamu wote: jambo hili lilishuhudiwa kwa wakati wake ufaao.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Timotheo 6:17-20 (NENO)*

# Watajipatia uzima, yaani, ule uzima ambao ni wa kweli... linda kile kilichowekwa amana kwako



**Waagize wale ambao ni matajiri wa ulimwengu huu waache kujivuna, wala wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si ya hakika, bali waweke tumaini lao katika Mungu ambaye hutupatia vitu vyote kwa wingi ili tuvifurahie. Waagize watende mema, wawe matajiri katika matendo mema, pia wawe wakarimu na walio tayari kushiriki mali zao na wengine. Kwa njia hii watajiwekea hazina kama msingi kwa ajili ya wakati ujao na hivyo watajipatia uzima, yaani, ule uzima ambao ni wa kweli. Timotheo, linda kile kilichowekwa amana kwako. Epuka majadiliano yasiyo ya utauwa na mabishano ambayo kwa uongo huitwa elimu,**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*2 Timotheo 1:9-10, 13-14 (NENO)*

# Alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu... Shika kwa uthabiti kielelezo cha mafundisho yenye uzima yale uliyoyasikia kwangu

---

**ambaye alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu: si kwa kadiri ya matendo yetu mema bali kwa sababu ya kusudi lake mwenyewe na neema yake. Neema hii tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele. Lakini sasa imefunuliwa kwa kudhihirishwa kwake Mwokozi wetu, Kristo Yesu, ambaye amebatilisha mauti na kuleta uzima na kutokufa kwa njia ya Injili. ... Shika kwa uthabiti kielelezo cha mafundisho yenye uzima yale uliyoyasikia kwangu, pamoja na imani na upendo katika Kristo Yesu. Ilinde ile amana uliyokabidhiwa kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

# Kila Andiko limevuviwa na Mungu... kwa kuwafundisha katika haki

**Kila Andiko limevuviwa na Mungu na lafaa kwa mafundisho, kwa kuwaonya watu makosa yao, kwa kuwaongoza na kwa kuwafundisha katika haki, ili mtu wa Mungu awe amekamilishwa, apate kutenda kila kazi njema. ... Nasi tunalo pia neno la hakika zaidi la unabii, ambalo mtafanya vyema mkiliangalia kwa bidii, kama vile nuru inavyong'aa gizani, hadi kupambazuka na nyota ya asubuhi izuke mioyoni mwenu. Zaidi ya yote, yawapasa mjue kwamba hakuna unabii katika Maandiko uliofasiriwa kama alivyopenda nabii mwenyewe. Kwa maana unabii haukuja kamwe kwa mapenzi ya mwanadamu, bali watu walinena yaliyotoka kwa Mungu wakiongozwa na Roho Mtakatifu.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 1:17, 19-22 (NENO)*

# Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu... mkalipokee kwa unyenyekevu lile Neno lililopandwa ndani yenu



**Kila kitolewacho kilicho chema na kilicho kamili, hutoka juu, na hushuka kutoka kwa Baba wa mianga, ambaye kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeukageuka. ... Ndugu zangu wapendwa, fahamuni jambo hili: Kila mtu awe mwepesi wa kusikiliza, lakini asiwe mwepesi wa kusema wala wa kukasirika. Kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Kwa hiyo, ondoleeni mbali uchafu wote na uovu ambao umezidi kuwa mwingi, mkalipokee kwa unyenyekevu lile Neno lililopandwa ndani yenu ambalo laweza kuokoa nafsi zenu. Basi kuweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 4:4, 6-8, 10, 12 (NENO)*

# Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema... Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi... Jinyenyekezeni mbele za Bwana, naye atawainua



**Ninyi wanaume na wanawake wazinzi, hamjui ya kwamba urafiki na dunia ni uadui na Mungu? Kwa hiyo mtu yeyote anayetaka kuwa rafiki wa dunia hufanyika adui wa Mungu. ... Lakini yeye hutupatia neema zaidi. Hii ndiyo sababu Andiko husema: "Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema." Basi mtiini Mungu. Mpingeni ibilisi, naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu ninyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu ninyi wenye nia mbili. ... Jinyenyekezeni mbele za Bwana, naye atawainua. ... Yuko Mtoa sheria mmoja tu na yeye peke yake ndiye Hakimu, ndiye awezaye kuokoa au kuangamiza. Lakini wewe ni nani hata umhukumu jirani yako?**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yakobo 4:13-17 (NENO)*

# Hamjui hata litakalotukia kesho... Kama Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili ama lile... Kujisifu kwa namna hiyo ni uovu



Basi sikilizeni ninyi msemao, “Leo au kesho tutakwenda katika mji huu ama ule tukae humo mwaka mmoja, tufanye biashara na kupata faida.” Lakini hamjui hata litakalotukia kesho. Maisha yenu ni nini? Ninyi ni ukungu ambao huonekana kwa kitambo kidogo kisha hutoweka. Badala yake, inawapasa kusema, “Kama Bwana akipenda, tutaishi na kufanya hili ama lile.” Kama ilivyo sasa, mnajisifu na kujigamba. Kujisifu kwa namna hiyo ni uovu. Basi mtu yeyote anayejua jema limpasalo kutenda, lakini asilitende, mtu huyo anatenda dhambi.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yuda 1:1-2, 20-21, 24-25 (NENO)*

# Rehema, amani na upendo viwe kwenu kwa wingi... ninyi wapendwa, jijengeni katika imani yenu iliyo takatifu sana

---

**Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo na nduguye Yakobo: Kwa wale walioitwa, wapendwa katika Mungu Baba na kuhifadhiwa salama ndani ya Yesu Kristo: Rehema, amani na upendo viwe kwenu kwa wingi. ... Lakini ninyi wapendwa, jijengeni katika imani yenu iliyo takatifu sana tena ombeni katika Roho Mtakatifu. Jilindeni katika upendo wa Mungu mkitazamia kwa furaha rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo ili awalete katika uzima wa milele. ... Kwake yeye awezaye kuwalinda ninyi msianguke na kuwaleta mbele za utukufu wake mkuu bila dosari na kwa furaha ipitayo kiasi: kwake yeye Mungu pekee Mwokozi wetu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu, utukufu, ukuu, uweza na mamlaka ni vyake tangu milele, sasa na hata milele! Amen.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Kutoka 20:2-8, 12-17, 20 (NENO)*

# Mimi ndimi Bwana Mungu wako… Usiwe na miungu mingine ila mimi… ninaonyesha upendo kwa maelfu ya vizazi vya wale wanipendao

“Mimi ndimi Bwana Mungu wako, niliyekutoa Misri, kutoka nchi ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi. Usijitengenezee sanamu katika umbo la kitu chochote kilicho juu mbinguni, au duniani chini, au ndani ya maji. Usivisujudie wala kuviabudu; kwa kuwa Mimi, Bwana Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu, ninayewaadhibu watoto kwa ajili ya dhambi za baba zao hadi kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, lakini ninaonyesha upendo kwa maelfu ya vizazi vya wale wanipendao na kuzishika amri zangu. Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako, kwa kuwa Bwana hataacha kumhesabia hatia yeye alitajaye jina lake bure. Ikumbuke siku ya Sabato, uitakase. … Waheshimu baba yako na mama yako, ili upate kuishi siku nyingi katika nchi anayokupa Bwana Mungu wako. Usiue. Usizini. Usiibe. Usimshuhudie jirani yako uongo. Usiitamani nyumba ya jirani yako. Usimtamani mke wa jirani yako, wala mtumishi wake wa kiume au wa kike, wala ng’ombe wake au punda wake, wala chochote kile alicho nacho jirani yako.” … Mose akawaambia watu, “Msiogope! Mungu amekuja kuwajaribu, ili kwamba hofu ya Mungu iwakalie, msitende dhambi.”



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yoshua 1:7-11 (NENO)*

# Uwe hodari na uwe na ushujaa mwingi... yatafakari maneno yake usiku na mchana... Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe kokote uendako

Uwe hodari na uwe na ushujaa mwingi. Uwe na bidii kutii sheria yote aliyokupa Mose mtumishi wangu, usiiache kwa kugeuka kuelekea kuume au kushoto, ili upate kufanikiwa popote uendako. Usiache Kitabu hiki cha Sheria kiondoke kinywani mwako; yatafakari maneno yake usiku na mchana, ili upate kuwa mwangalifu kufanya kila kitu sawasawa na yote yaliyoandikwa ndani yake. Ndipo utakapofanikiwa na kisha utastawi. Je, si mimi niliyekuamuru? Uwe hodari na shujaa. Usihofu wala usivunjike moyo, kwa kuwa Bwana Mungu wako atakuwa pamoja nawe kokote uendako." Ndipo Yoshua akawaagiza maafisa wa watu akisema, "Pitieni katika kambi yote mkawaambie watu, 'Wekeni tayari mahitaji yenu. Siku tatu kuanzia sasa mtavuka hii Yordani ili kuingia na kuimiliki nchi ambayo Bwana Mungu wenu anawapa iwe yenu wenyewe.'"



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*1 Samweli 16:7; 2 Samweli 7:18, 13, 23, 22 (NENO)*

# Mwanadamu hutazama katika sura ya nje, lakini Bwana hutazama moyoni

---

**Lakini Bwana akamwambia Samweli, “Usitazame sura yake wala kimo chake, kwa kuwa nimemkataa. Bwana hatazami katika vile vitu mwanadamu avitazamavyo. Mwanadamu hutazama katika sura ya nje, lakini Bwana hutazama moyoni.” … Ndipo Mfalme Daudi akaingia ndani, akaketi mbele za Bwana, akasema: “Ee Bwana Mwenyezi, mimi ni nani, na jamaa yangu ni nini, hata umenileta mpaka hapa nilipo? … Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa ajili ya Jina langu, nami nitaimarisha kiti cha enzi cha ufalme wake milele. … Naye ni nani aliye kama watu wako Israeli, taifa pekee duniani ambalo Mungu alitoka kwenda kulikomboa kwa ajili yake mwenyewe, na kujifanyia jina mwenyewe, kwa kufanya maajabu makubwa na ya kutisha kwa kuwafukuza mataifa na miungu yao mbele ya watu wako, ambao uliwakomboa kutoka Misri? … “Tazama jinsi ulivyo mkuu, Ee Bwana Mwenyezi! Hakuna mwingine kama wewe, wala hakuna Mungu ila wewe, kama vile tulivyosikia kwa masikio yetu wenyewe,**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Nehemia 1:4-11 (NENO)*

# Ambaye hulishika agano lake la upendo na wale wampendao... Ninaungama dhambi zetu sisi Waisraeli... Tumetenda uovu sana mbele zako

**Niliposikia mambo haya, niliketi, nikalia. Kwa siku kadhaa niliomboleza na kufunga na kuomba mbele za Mungu wa mbinguni. Kisha nikasema: "Ee Bwana, Mungu wa mbinguni, mkuu na mwenye kuogofya, ambaye hulishika agano lake la upendo na wale wampendao na kutii amri zake, tega masikio yako, na ufungue macho yako, ili usikie maombi ya mtumishi wako anayoomba mbele yako usiku na mchana kwa ajili ya watumishi wako, watu wa Israeli. Ninaungama dhambi zetu sisi Waisraeli, pamoja na zangu na za nyumba ya baba yangu, tulizotenda dhidi yako. Tumetenda uovu sana mbele zako. Hatukutii amri, maagizo na sheria ulizompa Mose mtumishi wako. "Kumbuka agizo ulilompa Mose mtumishi wako, ukisema, 'Kama mkikosa uaminifu, nitawatawanya miongoni mwa mataifa, lakini mkinirudia na kutii amri zangu, ndipo hata kama watu wenu walio uhamishoni wako mbali sana katika miisho ya dunia, nitawakusanya kutoka huko na kuwaleta mahali ambapo nimepachagua kuwa makao kwa ajili ya Jina langu.' "Hawa ni watumishi wako na watu wako, uliowakomboa kwa nguvu zako kuu na mkono wako wenye nguvu. Ee Bwana, tega sikio lako na usikie maombi ya huyu mtumishi wako, na maombi ya watumishi wako wanaofurahia kuliheshimu Jina lako. Nipe leo, mimi mtumishi wako, mafanikio kwa kunipa kibali mbele ya mtu huyu." Kwa maana nilikuwa mnyweshaji wa mfalme.**





*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

# Bwana huziangalia njia za mwenye haki, bali njia ya waovu itaangamia




**Heri mtu yule ambaye haendi katika shauri la watu waovu, wala hasimami katika njia ya wenye dhambi, au kuketi katika baraza la wenye mizaha. Bali huifurahia sheria ya Bwana, naye huitafakari hiyo sheria usiku na mchana. Mtu huyo ni kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao huzaa matunda kwa majira yake na majani yake hayanyauki. Lolote afanyalo hufanikiwa. Sivyo walivyo waovu! Wao ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. Kwa hiyo waovu hawatastahimili hukumu, wala wenye dhambi katika kusanyiko la wenye haki. Kwa maana Bwana huziangalia njia za mwenye haki, bali njia ya waovu itaangamia.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 4:1-8 (NENO)*

# Bwana amewatenga wale wamchao kwa ajili yake... Nitajilaza chini na kulala kwa amani, kwa kuwa wewe peke yako, Ee Bwana, waniwezesha kukaa kwa salama




**Nijibu nikuitapo, Ee Mungu wangu mwenye haki! Nipumzishe katika shida zangu; nirehemu, usikie ombi langu. Enyi watu, mtabadilisha utukufu wangu kuwa aibu mpaka lini? Mtapenda udanganyifu na kufuata miungu ya uongo mpaka lini? Fahamuni hakika kwamba Bwana amewatenga wale wamchao kwa ajili yake; Bwana atanisikia nimwitapo. Katika hasira yako, usitende dhambi. Mkiwa vitandani mwenu, mtulie kimya mkiichunguza mioyo yenu. Toeni dhabihu zilizo haki; mtegemeeni Bwana. Wengi wanauliza, "Ni nani awezaye kutuonyesha jema lolote?" Ee Bwana, tuangazie nuru ya uso wako. Wewe umejaza moyo wangu kwa furaha kubwa kuliko watu waliopata nafaka na divai kwa wingi. Nitajilaza chini na kulala kwa amani, kwa kuwa wewe peke yako, Ee Bwana, waniwezesha kukaa kwa salama.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 15:1-5 (NENO)*

# Ni yule aendaye pasipo mawaa, atendaye yaliyo haki... asemaye kweli toka moyoni mwake... Mtu afanyaye haya kamwe hatatikisika



**Bwana, ni nani awezaye kukaa katika Hekalu lako? Nani awezaye kuishi katika mlima wako mtakatifu? Ni yule aendaye pasipo mawaa, atendaye yaliyo haki, asemaye kweli toka moyoni mwake, na hana masingizio ulimini mwake, asiyemtenda jirani yake vibaya, na asiyemsingizia mwenzake, ambaye humdharau mtu mbaya, lakini huwaheshimu wale wamwogopao Bwana, yule atunzaye kiapo chake hata kama anaumia. Yeye akopeshaye fedha yake bila riba, na hapokei rushwa dhidi ya mtu asiye na hatia. Mtu afanyaye haya kamwe hatatikisika.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 13:1-3, 5-6 (NENO)*

# Ninategemea upendo wako usiokoma... Nitamwimbia Bwana, kwa kuwa amekuwa mwema kwangu



**Mpaka lini, Ee Bwana? Je, utanisahau milele? Utanificha uso wako mpaka lini? Nitapambana na mawazo yangu mpaka lini, na kila siku kuwa na majonzi moyoni mwangu? Adui zangu watanishinda mpaka lini? Nitazame, unijibu, Ee Bwana Mungu wangu. Yatie nuru macho yangu, ama sivyo nitalala usingizi wa mauti. ... Lakini ninategemea upendo wako usiokoma; moyo wangu unashangilia katika wokovu wako. Nitamwimbia Bwana, kwa kuwa amekuwa mwema kwangu.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 16:1-5, 7-11 (NENO)*

# Bwana umeniwekea fungu langu na kikombe changu... umeyafanya mambo yangu yote yawe salama... Umenijulisha njia ya uzima

---

**Ee Mungu, uniweke salama, kwa maana kwako nimekimbilia. Nilimwambia Bwana, “Wewe ndiwe Bwana wangu; pasipo wewe sina jambo jema.” Kwa habari ya watakatifu walioko duniani, ndio walio wa fahari ambao ninapendezwa nao. Huzuni itaongezeka kwa wale wanaokimbilia miungu mingine. Sitazimimina sadaka zao za damu au kutaja majina yao midomoni mwangu. Bwana umeniwekea fungu langu na kikombe changu; umeyafanya mambo yangu yote yawe salama. ... Nitamsifu Bwana ambaye hunishauri, hata wakati wa usiku moyo wangu hunifundisha. Nimemweka Bwana mbele yangu daima. Kwa sababu yuko mkono wangu wa kuume, sitatikisika. Kwa hiyo moyo wangu unafurahia, na ulimi wangu unashangilia; mwili wangu nao utapumzika salama, kwa maana hutaniacha kaburini, wala hutamwacha Mtakatifu Wako kuona uharibifu. Umenijulisha njia ya uzima; utanijaza na furaha mbele zako, pamoja na furaha za milele katika mkono wako wa kuume.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Zaburi 23:1-6 (NENO)*

# Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu... hunihuisha nafsi yangu... wewe upo pamoja nami



Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Hunilaza katika malisho ya majani mabichi, kando ya maji matulivu huniongoza, hunihuisha nafsi yangu. Huniongoza katika njia za haki kwa ajili ya jina lake. Hata kama nikipita katikati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya, kwa maana wewe upo pamoja nami; fimbo yako na mkongojo wako vyanifariji. Waandaa meza mbele yangu machoni pa adui zangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, kikombe changu kinafurika. Hakika wema na upendo vitanifuata siku zote za maisha yangu, nami nitakaa nyumbani mwa Bwana milele.



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Mithali 1:7; 9:18; 4:23-26 (NENO)*

# Linda moyo wako, kuliko yote uyalindayo, maana ndiko zitokako chemchemi za uzima

---

**Kumcha Bwana ndicho chanzo cha maarifa, lakini wapumbavu hudharau hekima na adabu. ... Lakini hawajui hata kidogo kuwa wafu wako humo, kwamba wageni wake huyo mwanamke wako katika vilindi vya kuzimu. ... Zaidi ya yote, linda moyo wako, kuliko yote uyalindayo, maana ndiko zitokako chemchemi za uzima. Epusha kinywa chako na ukaidi; weka mazungumzo machafu mbali na midomo yako. Macho yako na yatazame mbele, kaza macho yako moja kwa moja mbele yako. Sawazisha mapito ya miguu yako na njia zako zote ziwe zimethibitika.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yeremia 17:5, 7-10 (NENO)*

# Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi... Mimi Bwana huchunguza moyo na kuzijaribu nia

---

**Hili ndilo asemalo Bwana: "Amelaaniwa yeye amtegemeaye mwanadamu, ategemeaye mwenye mwili kwa ajili ya nguvu zake, ambaye moyo wake umemwacha Bwana. ... "Lakini amebarikiwa mtu ambaye tumaini lake ni katika Bwana, ambaye matumaini yake ni katika Bwana. Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji uenezao mizizi yake karibu na kijito cha maji. Hauogopi wakati wa joto ujapo; majani yake ni mabichi daima. Hauna hofu katika mwaka wa ukame na hautaacha kuzaa matunda." Moyo ni mdanganyifu kuliko vitu vyote, ni mwovu kupita kiasi. Ni nani awezaye kuujua? "Mimi Bwana huchunguza moyo na kuzijaribu nia, ili kumlipa mtu kwa kadiri ya mwenendo wake, kwa kadiri ya matendo yake yanavyostahili."**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Yoeli 2:11-14 (NENO)*

# Nirudieni kwa mioyo yenu yote, kwa kufunga, kwa kulia na kuomboleza... yeye ndiye mwenye neema na mwingi wa huruma, si mwepesi wa hasira

---

**Siku ya Bwana ni kuu, ni ya kutisha. Ni nani anayeweza kuistahimili? "Hata sasa," asema Bwana, "nirudieni kwa mioyo yenu yote, kwa kufunga, kwa kulia na kuomboleza." Rarueni mioyo yenu na siyo mavazi yenu. Mrudieni Bwana, Mungu wenu, kwa maana yeye ndiye mwenye neema na mwingi wa huruma, si mwepesi wa hasira, ni mwingi wa upendo, huona huruma, hujizuia kuleta maafa. Ni nani ajuaye? Yeye aweza kugeuka na kuwa na huruma na kuacha baraka nyuma yake: sadaka za nafaka na sadaka za vinywaji kwa ajili ya Bwana Mungu wenu.**



*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Obadia 1:3-4, 15, 17 (NENO)*

# Kiburi cha moyo wako kimekudanganya... Kama ulivyofanya, nawe utafanyiwa vivyo hivyo



**Kiburi cha moyo wako kimekudanganya, wewe unayeishi katika majabali ya miamba na kufanya makao yako juu, wewe unayejiambia mwenyewe, 'Ni nani awezaye kunishusha chini?' Ingawa unapaa juu kama tai na kufanya kiota chako kati ya nyota, nitakushusha chini kutoka huko," asema Bwana. ... "Siku ya Bwana iko karibu kwa mataifa yote. Kama ulivyofanya, nawe utafanyiwa vivyo hivyo, matendo yako yatakurudia juu ya kichwa chako. ... Lakini katika Mlima Sayuni kutakuwepo na wale watakaookoka; nao utakuwa mtakatifu, nayo nyumba ya Yakobo itamiliki urithi wake.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Nahumu 1:2-3, 5, 7 (NENO)*

# Bwana ni Mwema, kimbilio wakati wa taabu. Huwatunza wale wanaomtegemea

---

**Bwana ni mwenye wivu na Mungu mlipiza kisasi; Bwana hulipiza kisasi na amejaa ghadhabu. Bwana hulipiza kisasi juu ya watesi wake, naye anadumisha ghadhabu yake dhidi ya adui zake. Bwana si mwepesi wa hasira naye ni mwenye nguvu, Bwana hataacha kuadhibu wenye hatia. Njia yake ipo katika kisulisuli na tufani, na mawingu ni vumbi la miguu yake. ... Milima hutikisika mbele yake na vilima huyeyuka. Nchi hutetemeka mbele yake, dunia na wote waishio ndani yake. ... Bwana ni Mwema, kimbilio wakati wa taabu. Huwatunza wale wanaomtegemea,**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*

*Mika 6:6, 8; Habakuki 2:4-5 (NENO)*

# Kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako... mwenye haki ataishi kwa imani yake



**Nimjie Bwana na kitu gani na kusujudu mbele za Mungu aliyetukuka? Je, nije mbele zake na sadaka za kuteketezwa, nije na ndama za mwaka mmoja? ... Amekuonyesha yaliyo mema, ee mwanadamu. Bwana anataka nini kwako? Ila kutenda kwa haki na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako. ... "Tazama, amejaa majivuno; anavyovitamani si vya unyofu: lakini mwenye haki ataishi kwa imani yake: hakika mvinyo humsaliti; ni mwenye kiburi na hana amani. Kwa sababu ni mlafi kama kuzimu na kama kifo kamwe hatosheki; anajikusanyia mataifa yote na kuchukua watu wote mateka.**

***Spiritual Warfare Cards.com***

*Neno: Bibilia Takatifu · CC BY-SA 4.0 · Biblica, Inc.*